**Maswali na Majibu**

1. Watu walikuwa namna gani kwa siku za Nuhu?
   *Walikuwa waovu na wajeuri, hawakupenda Mungu*.
2. Mbona Mungu alifurahia Nuhu?
   *Nuhu alimpenda Mungu na alijaribu kumfurahisha*.
3. Nuhu angeheba uharibivu wa Mungu kwa watu waovu namna gani?
   *Kwa kumtii Mungu na ajenge safina*.
4. Watu waliambia Nuhu eti nini alipokuwa akijenga safina?
   *Yeye ni mjinga, hakutakuwa na gharika*.
5. Nani alifunga mlango wa safina? *Mungu.*
6. Nani aliokoka kutoka kwa gharika?
   *Nuhu, mkewe, wana wao 3 na wake wao na wanyama waliokuwa kwa safina*.
7. Nuhu alijuaje kwamba gharika ilikuwa imekauka?
   *Alituma kunguru na njiwa wawili.*
8. Nuhu alifanya nini kama shukrani kwa Mungu alipotoka nje ya safina?
   *Alijenga madhabahu na akatolea Mungu dhabihu*.
9. Ahadi mbili zenye Mungu aliahidi Nuhu ni gani?
   *Hataleta gharika duniani tena, na majira ya anga itaendelea kuweko*.
10. Tunajifunza nini kwa ulevi wa Nuhu?
    *Ulevi unasababisha tabia sizofaa, kwa hivyo tusilewe*.
11. Agano ni nini? *Ahadi ya masharti. Ukifanya hivi …. HALAFU Mungu ata ….*
12. Gharika ni picha ya ubatizo namna gani?
    *Nuhu aliokoka kwa kifo kwa njia ya maji. Ubatizo unatuokoa kupitia kwa maji.*

### Mistari ya kukariri

1 Peter 3:20 – 21

### Mazungumzo

Hizi mistari zinatufundisha nini juu ya ulevi? Waefeso 5:18 na Mithali 23:20 – 21

### Kuandika

Eleza vile gharika ni picha ya ubatizo.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 6 Nuhu na gharika


**SOMA Mwanzo milango ya 6, 7 na 8**

**SOMO**

**Watu walikuwa waovu** Adamu na Hawa walipata watoto na wajukuu. Hatimaye dunia ikawa na watu wengi na hao watu wakawa waovu. Wakawa wabaya, wenye jeuri na hawakupenda Mungu. Kila mtu alikuwa muovu sana mpaka Mungu akasikitika kwa kumuumba mtu. Mungu akaamua kwamba itakuwa vyema kuanza tena.

**Familia moja iliyokuwa njema** Mtu mmoja alipenda Mungu na alijaribu kumfurahisha Mungu. Jina lake lilikuwa Nuhu. Mungu alifurahia Nuhu sana. Mungu akamwambia vile atamhebesha kutoka kwa uharibivu atakaouletea watu waovu. Mungu alimwambia ajenge mashua kubwa itwayo safina.

Nuhu alikuwa aamue mwenyewe. Angeamua kuamini Mungu na amtii. Au angekataa na awe kama watu wengine na asahahu Mungu. Haikukuwa rahisi vile, kuamini Mungu na ajenge mashua kubwa katikati ya nchi. Watu walimcheka na kumwambia kwamba yeye ni mjinga. Walisema kwamba hakutakuwa na gharika. Lakini Nuhu aliamini Mungu na akaendelea vile Mungu alikuwa ameamrisha. Nuhu na familia yake walijenga safina.



**Gharika ilikuja** Nuhu hakukuwa mjinga. Gharika ya maji ilikuja. Siku moja Mungu aliaambia Nuhu pamoja na familia yake (mke wa Nuhu, wana wake 3 na wake wao) kuenda ndani ya safina. Nuhu alichukuwa hata wanyama kwa safina. Alichukuwa wawili kwa kila aina lakini wanaoliwa, alichukuwa saba saba kwa kila aina vile Mungu alikuwa ameamrisha. Halafu Mungu akafunga mlango wa safina.

Mungu alituma dhoruba na mawimbi ya nguvu kutoka kwa bahari. Maji yalizambaa nchi yote. Watu wote na wanyama waliangamizwa kwa gharika. Nuhu, familia yake, wanyama aliokuwa nao katika safina ndio walipona.

Mvua ilinyesha kwa wiki sita. Baadaye maji yalianza kupungua. Baada ya miezi tano safina ilitua juu ya mlima. Nuhu alingoja kwa utulivu ili nchi ikauke.

Nuhu alituma ndege waende waangalie kama maji yamekauka. Kwanza alituma kunguru lakini hakurudi kwa vile alikuwa na nguvu za kupuruka angani kwa muda bila kutua. Baadaye alituma njiwa, alirudi kwa sababu hakukuwa na mahali pa kutua. Wiki moja ilipoisha, Nuhu alituma njiwa tena. Mara hii njiwa alikuja na jani mbichi la mzeituni mdomoni mwake. Hapo Nuhu alijua kwamba maji yalikuwa yanaendelea kukauka na miti zimeanza kukua

Nuhu na familia yake walikaa kwa safina muda wa karibu mwaka mmoja. Halafu Mungu alifungua mlango na wakatoka nje kwa ulimwengu uliokuwa tupu. Mungu alianzisha uzao mpya wa wanadamu. Nuhu aliokoka kwa sababu aliamini Mungu na kumtii. Mungu aliambia Nuhu na familia yake wazae na wajaze dunia tena.

**Mungu anapea Nuhu na familia yake ahadi** Nuhu alitaka kumshukuru Mungu kwa kumweka yeye na familia yake kuwa hai na kuanzisha uzao mpya. Nuhu alijenga madhabahu. Aliua wanyama fulani na kuchoma ili kumtolea Mungu kama dhabihu. Hawa wanyama walikuwa wa maana sana kwa Nuhu lakini aliamua kumtolea Mungu kama shukrani na kumwabudu. Njia hii ya dhabihu ni kama ibada. Wakati huu hatuui mnyama ili tumtolea Mungu dhabihu. Lakini inatupasa tuwe tayari kumpa Mungu vitu vyetu, tumpende na kumtii.

Nuhu alipotolea Mungu dhabihu, Mungu alimpa ahadi. Mungu alitarajia kwamba watu watampenda na kumtii. Mungu aliahidi vitu viwili:

* Hata haribu tena dunia kwa gharika.
* kupanda na kuvuna, baridi na joto, kaskazi na kusi, mchana na usiku vitakuweko milele.

Mungu alitengeneza upinde angani. Alisema kwamba upinde wa mvua ni ishara ya kukumbusha ahadi yake kwamba hatagharikisha dunia tena. Tukiona upinde, tunakumbuka hiyo gharika na vile Nuhu aliokolewa. Tunakumbuka kwamba Mungu angali anatimiza ahadi yake kwa Nuhu.





**Nuhu analewa** Baada ya maji ya gharika kuisha, Nuhu alipanda shamba la mizabibu. Shamba la mizabibu ni pahali mizabibu inapandwa. (Zabibu huwa zinakua kwa mzabibu na zinatumiwa kutengeneza divai). Nuhu alitengeneza divai na akanywa. Alilewa na akafanya vyenye hakuwa akielewa. Alilala uchi katika hema yake. Mwanawe, Hamu alikuja na akampata amelala uchi halafu akaenda nje na kuambia ndugu zake wawili, Shemu na Yafethi. Shemu na Yafethi walichukuwa vazi na kuenda kinyumenyume na kumfunika baba yao bila kuona uchi wake. Kwa sababu si vyema watoto kuona uchi wa baba yao.

Nuhu alikuwa mtu aliyekuwa mwema lakini alifanya kosa. Ubaya wa vileo kama divai na pombe, ni kwamba, vinalewesha haraka sana. Mtu mlevi si rahisi kujizuia kufanya mambo yasiyofaa – kama Nuhu. Kwa hivyo tusilewe kwa kunywa vileo. Tukilewa tunaweza kufanya makosa makubwa na kusini zaidi.

**Agano** Ahadi zilizo fanywa kwa Nuhu zinaitwa agano. Hili neno limetumika sana kwa Biblia na linamaanisha ahadi. Agano ni ahadi yenye masharti. Mungu anaahidi kwamba kitu fulani kitafanyika kama watu watamtii.

**Ubatizo (1 Petro 3:20 – 21)** Nuhu na gharika ni mfano wa ubatizo.






| | |
|---|---|
| **Nuhu aliamini Mungu na akafanya vile Mungu alisema. Alijenga safina.** | **Tunaamini Mungu na tunamtii.** |
| Nuhu alitoka kwa dunia ya uovu. Alienda kwa safina. | Tunakataa kuishi kama dunia ya uovu na kuenda kwa maji ya ubatizo. |
| **Wakati wa gharika, safina ilizungukwa kwa maji. Maji yalikuwa chini na mvua ikawa juu.** | **Tunaingia ndani ya maji ya ubatizo na tunazungukwa kwa maji.** |
| Nuhu alitoka inje ya safina na kuanza | Tunatoka ndani ya maji na kuanza maisha mapya ya kufurahisha Mungu. |
| **Nuhu aliokoka kutoka kwa gharika** | **Mungu anatuokoa kwa kututakia maisha ya milele** |